

## **Dhima ya Usasanyuzi Dosari katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha ya Pili: Mifano ya Wajifunzaji wa Kiswahili katika Jamii ya Wakinga Nchini Tanzania**

Arnold B. G. Msigwa  
Chuo Kikuu cha Kabale  
agmsigwa@kab.ac.ug

### **Ikisiri**

*Usasanyuzi dosari ni eneo muhimu katika taaluma ya isimu tumizi. Vilevile, ni mbinu pangilifu ya kuchanganua dosari za mjifunzaji lugha. Kitaaluma dosari si kitu kibaya bali ni kipengele muhimu sana katika mchakato wa ujifunzaji lugha. Dosari husaidia kutambua mchakato changamani wa maendeleo ya lugha na namna pangilifu ya kubaini, kueleza na kufafanua dosari za mjifunzaji lugha. Pia, dosari zinaweza kusaidia kutoa welewa wa mchakato wa kuamili Lugha ya pili. Makala haya, kwa hiyo, yanalenga: kubainisha dosari zinazojitokeza kwa wajifunzaji wa Kiswahili katika jamii ya Wakinga, sababu za wajifunzaji wa lugha ya pili katika jamii ya Wakinga na kupendekeza mikakati ya kupunguza hizo dosari. Baadhi ya dosari zilizobainika ni dosari za undoshaji wa fonimu /h/, uchopekaji wa fonimu /u/ na dosari za kimuundo; yaani ukosefu wa upatanisho wa kisarafu. Dosari hizi za uchopekaji zimesababishwa na uhawilishaji wa kanuni za lugha ya kwanza katika lugha ya Kiswahili; ambapo mjifunzaji wa lugha ya pili amehamisha utaratibu wa lugha yake ya kwanza na kuutumia kwenye lugha ya pili anayojifunza na kusababisha dosari. Aina hii ya uhawilishaji ni uhawilishaji hasi. Makala yanahitimisha kwamba dosari hizi zinachangiwa kwa kiasi kikubwa na lugha yao ya kwanza.*

**Maneno Muhimu:** dosari, usasanyizi dosari na uhawilishaji.

### **1.0 Utangulizi**

Usasanyuzi dosari ni kipengele muhimu katika taaluma ya Isimu Tumizi

na katika ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya pili. Isimu Tumizi ni taaluma inayoshughulikia changamoto na matatizo mbalimbali yanayohusiana na ufundishaji na uamiliaji wa lugha. Pia, taaluma hii inajaribu kutafuta majawabu ya changamoto hizi ili kuwezesha ujifunzaji na ufundishaji lugha kuwa wenye tija. Usasanyuzi dosari unaibua ufahamu wa kina wa mchakato wa ufundishaji wa lugha. Zipo tafiti kadhaa (kwa mfano: Darus, 2009; Ellis, 1995; James, 1989; Keshavarz, 2003, 2006; Norrish, 1983; Ziahisseiny, 1999) zilizofanywa na zenye kuonesha mwelekeo wa usasanyuzi dosari na ufahamu wa kina kuhusiana na ujifunzaji na uamiliaji wa lugha.

Matokeo ya tafiti hizi yametumika kwa kipindi kirefu katika ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya pili. Kwa mujibu wa Corder (1967, 1971 & 1974) inadhaniwa kwamba wajifunzaji wa lugha ya pili wanajifunza lugha hiyo karibu sawa na wanavyojifunza lugha ya kwanza. Hitimisho hili lilitokana na ukweli kwamba, watoto wanapoamili<sup>1</sup> lugha ya kwanza husababisha dosari na makosa mengi. Kutokana na dosari zinazofanywa na watoto, watafiti hawa wanabainisha kwamba, ujifunzaji wa lugha ya pili hufanyika sawasawa na ujifunzaji wa lugha ya kwanza. Aidha, Corder (1967) anaonesha tofauti kati ya dosari na makosa kama ifuatavyo:

Aidha, katika majaribio ya kufafanua suala la kasoro za wajifunzaji lugha, Corder anatumia istilahi mbili: dosari na makosa. *Dosari* ni matokeo ya ujifunzaji usiokamilifu wa kanuni za kiisimu kwa mjifunzaji lugha na kwamba dosari hizi haziwezi kurekibishwa na mjifunzaji lugha mwenyewe. *Makosa* kwa upande mwingine, ni matokeo ya utumizi

---

<sup>1</sup> Dhana hii ilipendekezwa na Krashan miaka ya 1970 ikiwa na maana ya mchakato wa kiisimu unaotokea kwa wajifunzaji wa lugha ya pili au ya Kigeni katika hali ya ung'amuzibwete. kwa maana ya kuwa, mjifunzaji lugha hung'amua kanuni za lugha pasipo kukusudia wala mwenyewe kufahamu kwamba jambo hilo linatokea.

mbaya wa kanuni za lugha kutokana na sababu mbalimbali kama vile uchovu, uzembe na kutojali kwa mjifunzaji. Ufafanuzi huu unamaanisha kwamba, makosa yanatokana na mjifunzaji mwenyewe, wakati dosari zinatokana na mbinu zilizotumika katika ufundishaji. Corder (keshatajwa) anaamini kuwa, dosari ziko nje ya mjifunzaji lugha mwenyewe ilhali, makosa yako ndani ya uwezo wa mjifunzaji. Hii inamaanisha kwamba, mjifunzaji anakuwa anafahamu vema kanuni na miundo ya lugha husika na anaweza kujirekebisha mwenyewe ikiwa uchovu, uzembe na kutojali havitakuwepo. Hii ndiyo tofauti ya msingi kati ya dosari na makosa. Hivyo, ili kufanya uchanganuzi sahihi mchanganuzi lazima awe na uhakika kuhusu utambuzi wa dosari zifanywazo na wajifunzaji wa lugha.

Katika hatua za awali za kuamili lugha kama wafanyavyo watoto wadogo, wajifunzaji pia huibua tungo ambazo siyo sahihi kisarufi na kisemantiki na baadaye kadiri wanavyoendelea kupata ingizo<sup>2</sup> kama vile mafunzo, maelekezo, ufafanuzi na mrejesho wanaanza kujirekebisha wenyewe. Wajifunzaji wa lugha ya pili pia hupitia hatua hii. Kimsingi, hakuna tofauti kati ya kuamili lugha ya kwanza na kujifunza lugha ya pili (Corder, 1967). Usasanyuzi dosari una dhima muhimu katika ufundishaji wa lugha ya pili. Usasanyuzi dosari huwasaidia walimu kufahamu njia mpya za kufundisha kwa kutoa mrejesho wa dosari zilizofanywa na wajifunzaji.

Aidha, inaeleweka na ni uhakika kwamba wajifunzaji lugha hufanya makosa katika mchakato wa kujifunza lugha. Dosari hizi zinatoa ufahamu mpya na mbinu za kufundishia kwa walimu wa lugha na wanaisimu katika kukabiliana na matatizo yenye kuhusiana na ufundishaji wa lugha. Kwa mujibu wa nadharia za Wanautabia, ujifunzaji wa lugha ni ujenzi na

---

<sup>2</sup> Ingizo ni tafsiri ya neno la Kiingereza “**input**” ikiwa na maana ya kitu chochote anachopata mjifunzaji wa Lugha ya pili au kigeni kwa kusikia, kuona, kunusa au kugusa ambacho kwa namna moja ama nyingine husaidia kuboresha uelewa wake kuhusu lugha anayojifunza.

uimarikaji wa tabia. Dosari katika ujifunzaji wa lugha ya pili zinatokana na ukosefu wa kanuni zilizotengenezwa wakati wa kujifunza lugha ya kwanza. Tabia hizi huibuka na kujengeka wakati wa mchakato wa kujifunza Lugha ya kwanza zinaingilia na kuathiri kuibuka na kujengeka kwa tabia katika kujifunza Lugha ya pili.

Kulingana na Wanautabia kama vile Skinner (1957), dosari za mjifunzaji wa lugha ni matokeo ya mwingiliano wa lugha ya kwanza. Lengo la Makala haya ni kubainisha dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili katika jamii ya Wakinga, kufafanua sababu za utokeaji wa dosari hizo na kupendekeza mbinu zinazoweza kusaidia kuepukana na dosari hizo. Utafiti mdogo uliofanywa kwa njia ya ushuhudiaji unaonesha kuwa, wajifunzaji wa Lugha ya pili katika jamii ya Wakinga hufanya dosari mbalimbali. Hata hivyo, chanzo cha hizo dosari hakifahamiki. Kwa hiyo, data za makala haya zilikusanywa kwa kutumia njia za uandishi wa insha na hojaji.

### **1.1 Usuli wa Kihistoria kuhusu Maendeleo ya Taaluma ya Usasanyuzi Dosari**

Kama ilivyodokezwa hapo juu, katika kipindi cha miaka ya 1940, usasanyuzi dosari ulichagizwa na ujifunzaji lugha ulioegemea katika nadharia za Wanautabia. Ilichukuliwa kuwa ujifunzaji lugha ni mchakato wa ujenzi na kuimarika kwa tabia, na kwamba tabia (kanuni) za lugha moja ikishaanza inasababisha ukinzania katika kujifunza tabia (kanuni) za lugha ya pili au ngeni. Usasanyuzi linganishi ulifanyika kwa kutazama dosari za mjifunzaji lugha kwa kutalii kanuni za lugha zote mbili. Ikiwa kulikuwa na ufanano baina ya kanuni au miundo ya lugha hizi mbili basi uhawilishaji chanya hutokea, yaani ukinzani hautokei na ikiwa kuna mwachano baina ya kanuni au miundo ya lugha hizi mbili, uhawilishaji

hasi hutokea kwa mjifunzaji; yaani ukinzania hutokea.

Kwa ujumla, katika kipindi cha miaka ya 1940 dosari za wajifunzaji lugha ya pili zilinasibishwa na athari za lugha ya kwanza (Ellis, 1995; Gass & Selinker, 2008; Kazemian & Hashemi, 2014; Norrish, 1983; Sanal, 2007). Hata hivyo, Nadharia ya Usasanyuzi Linganishi haikuweza kueleza sababu zote za dosari za mjifunzaji lugha. Kwa maana kwamba michakato ya dosari za mjifunzaji lugha ni changamani mno, kwani kuna baadhi ya mambo ambayo yapo nje ya lugha ya mjifunzaji.

## **1.2 Maswali ya Utafiti**

Makala haya yamejibu maswali yafuatayo:

- a) Dosari gani zinazofanywa na wajifunzaji wa lugha ya pili katika jamii ya Wakinga?
- b) Sababu zipi zinasababisha kutokea kwa dosari hizo kwa wajifunzaji wa lugha ya pili katika jamii ya Wakinga?
- c) Mbinu zipi zinaweza kusaidia kuondoa dosari miongoni mwa wajifunzaji wa lugha ya pili katika jamii ya Wakinga?

## **2.0 Mapitio ya Maandiko**

Mwanzoni kabisa, eneo la usasanyuzi dosari lilifungamanishwa na nadharia za ujifunzaji lugha za Wanautabia kama vile: Skinner (1957) na Lado (1957), japo kwa kutaja wachache. Wataalamu hao wanadai kuwa dosari za mjifunzaji ni matokeo ya kuwapo kwa mwingiliano wa kanuni kati ya lugha ya kwanza na lugha ya pili. Aidha, dosari za mjifunzaji zilihusishwa na taaluma ya usasanyuzi linganishi, ambayo ilikuwa inalinganisha mifumo ya lugha mbili kwa kuangalia zinavyofanana na

kutofautiana, kisha kufanya ubashiri wa kitu ambacho kitatokea kwa mjifunzaji lugha. Mhalani tuseme lugha X, ambayo ni tofauti na lugha tuseme Y anayojifunza. Miongoni mwa watafiti hao ni pamoja na Lado (1957). Baadaye kidogo, Corder (1967, 1974) alibaini wazi kwamba mwelekeo huu wa usasanyuzi linganishi ulishindwa kutoa maelezo toshelevu kuhusu dosari za mjifunzaji. Ilibainika wazi na watafiti mbalimbali kama vile Gawasike (2016), Wei (2008) na Gass na Selinker (2008) kwamba, dosari za mjifunzaji lugha hazitokani tu na mwingiliano baina ya Lugha ya kwanza ila masuala mbalimbali ya kimajumui kuhusiana na miundo ya lugha yaliyoelekea kusababisha dosari kwa wajifunzaji lugha.

## **2.1 Sababu Zinazopelekea Dosari kwa Wajifunzaji Lugha**

Zipo sababu mbalimbali za dosari miongoni mwa mjifunzaji lugha ya pili. Sababu mojawapo ya dosari za wajifunzaji lugha yaweza kuwa uhaba wa vifaa vya kujifunzia lugha au upungufu wa vifaa vya kufundishia kwa mwalimu. Miongoni mwa sababu nyingine zilizobainishwa na watafiti kama vile James (1989, 1998), Ellis (1995), Ziahosseiny (1999), Kashavarz (2003, 2006), Şanal (2007), Darus (2009), Kazemian & Hashemi (2014) kuhusu chanzo cha dosari kwa wajifunzaji lugha ni: (i) Uhawilishaji lugha, (ii)Ujumuiivuwa kanuni, (iii) Urahisishajiwa kanuni, (iv) sababu za Uepukaji, (v) Ukakamaaji, (vi) Kutokuwa na maarifa ya lugha, na (vii) Mwingiliano na lugha nyingine.

### **2.1.1 Uhawilishaji lugha**

Uhawilishaji lugha ni sababu inayotokea zaidi katika mazingira ya ujifunzaji wa lugha moja, kwa mfano, lugha ya pili ambapo mjifunzaji lugha huyu tayari anayo lugha nyingine mathalani lugha ya kwanza. Katika mazingira, hayo mjifunzaji lugha huyu huelekea kuhamisha

kanuni za lugha ya kwanza na kuzitumia katika lugha ya pili. Kwa lugha nyepesi, uhawilishaji ni hali ya mjifunzaji wa lugha ya pili kuhamisha kanuni na miundo ya lugha ya kwanza na kuitumia katika mfumo wa lugha ya pili. Uhawilishaji lugha hutokea kwa namna mbili: chanya na hasi. Ikiwa lugha mbili zinazohusika zinafanana kimuundo na kimfumo, uhawilishaji chanya unaweza kutokea; na pale ambapo mifumo ya lugha zinazohusika hutofautiana, uhawilishaji hasi hutokea. Kulingana na Selinker (1972), uhawilishaji lugha ni utumizi wa kanuni za lugha moja katika kujifunza lugha nyingine.

### **2.1.2 Ujumuiwu wa kanuni**

Ujumuiwu wa kanuni ni hali ambayo kanuni moja au mfumo mmoja wa lugha unajumuishwa katika mifumo mingine. Ni upanuaji wa matumizi ya kanuni moja katika mazingira ambapo yanaweza yasiwe kubalifu hujulikana kama *ujumuiwu*. Hii huwa ni chanzo cha dosari kwa wajifunzaji wa lugha ya pili au ya kigeni. Kwa mfano, wanafunzi wageni wanaojifunza lugha ya pili hufanya dosari zifuatazo:

#### **A. Lugha ya kwanza (Kiingereza)**

1. I am in Dar es Salaam.  
Salaam.
2. I am going to Arusha.  
Arusha.
3. I am not eating.

#### **B. Lugha ya pili**

- \* Nipo katika Dar es
- \* Ninakwenda cha/kwa
- \* Sikuli.

Dosari zilizobainishwa katika safu B ni mfano wa dosari za ujumuiwu wa kanuni za lugha ya kwanza. Mwanafunzi ametumia utaratibu wa Lugha ya kwanza katika lugha ya pili na kusababisha dosari. Akishadidia hili, James (1998) anaeleza kwamba hali hii pia hutokea kwa watoto wanapojifunza lugha ya kwanza.

### **2.1.3 Urahisishaji wa kanuni**

Urahisishaji wa Kanuni ni dosari zinazohusu mjifunzaji kukwepa kutumia kanuni changamani na kupendelea kutumia kanuni za kawaida na nyepesi. Mbinu hii pia hujulikana kama mbinu ya uepukaji. Hali hii ya mjifunzaji kukwepa kutumia kanuni na miundo changamani husababisha pelekea kufanya dosari. Kwa mfano, katika jamii ya Kihaya kuna changamoto ya kutamka silabi *ng'a* na *ha*. Hivyo, wajifunzaji na watumiaji wa lugha ya pili katika jamiilugha ya Wahaya, hukwepa matashi ya silabi hizo wanapozungumza lugha ya pili. Aidha, katika utafiti uliofanyika mwaka 2016 kuhusu wajifunzaji wa Lugha ya pili ikiwa ni lugha ya pili katika jamii ya Wakinga, walionekana kukwepa kutumia urejeshi unaojitokeza mwishoni mwa kitenzi na urejeshi unaotumia *amba*. Watoa taarifa wote walitumia namna moja tu ya kudhihirisha urejeshi katika Kiswahili. Kukwepa au kurahisisha huko kulisababisha dosari mbalimbali (taz. Gawasike, 2016).

### **2.1.4 Ukakamaaji**

Ukakamaaji ni dosari ambazo mjifunzaji wa Lugha ya pili au ya kigeni kushindwa kubadili dosari mbalimbali zilizokuwa zinafanywa kipindi cha *lugha darajia/lugha mpito*<sup>3</sup> licha ya maelekezo mbalimbali ayapatayo kutoka kwa walimu au licha ya kufundishwa na kuwa na fursa mbalimbali za kufanyia mazoezi. Han (2013) anaeleza kwamba, ukakamaaji ni dosari sugu anazozipata mjifunzaji wa lugha, ambazo haziwezi kubadilika au kurekebishwa. Dosari hizi zinaweza kujidhirisha katika viwango mbalimbali vya lugha, kuanzia kiwango cha sauti hadi kilongo (Wei, 2008). Katika utafiti uliofanyika miongoni mwa wajifunzaji wa lugha ya pili katika jamii ya Wakinga, dosari za ukakamaaji zinajitokeza katika

---

<sup>3</sup> Ni aiana ya lugha ambayo mjifunzaji wa lugha ya pili au ya kigeni hujiundia kabla ya kufikia umilisi wa lugha anayojifunza/amili. Kwa kawaida lugha darajia au lugha mpitio huambatana na dosari mbalimbali za kimuundo, kimaana na kimofolojia.



fonolojia na mofolojia.

### **2.1.5 Kutokuwa na maarifa ya lugha**

Kutokuwa na maarifa ya lugha, ni miongoni mwa sababu za dosari kwa wajifunzaji wa lugha ya pili. Wakati mwingine wajifunzaji lugha hufanya dosari kutokana na kukosa au kutojua kanuni za lugha husika. Ukosefu wa kanuni na maarifa ya lugha husababisha mjifunzaji kufanya dosari au makosa anapozungumza au kuandika lugha ya pili. Hali hii humkwamisha mjifunzaji lugha. Huu ni usuli kwa ufupisho kuhusu usasanyuzi dosari.

### **3.0 Kiunzi cha Nadharia**

Makala haya yaliongozwa na kiunzi cha Nadharia cha Usasanyuzi Dosari kama kilivyoasisiwa na Corder (1967) na kufanyiwa maboresho na Corder mwenyewe mwaka 1971. Usasanyuzi dosari ni uchanganuzi wa kiisimu, ambao umejikita katika kupambanua dosari za wajifunzaji wa lugha ya pili au lugha ya kigeni. Usasanyuzi dosari ni njia ya kuainisha, kupambanua na kufafanua dosari zinazofanywa na mtu anayejifunza lugha ya pili au Lgn. Hoja kuu ya Nadharia ya Usasanyuzi Dosari ni kuwa dosari za wajifunzaji wa lugha ya pili au Lgn hazitokani tu na athari za lugha ya kwanza kama wanausasanyuzi linganishi kama vile Lado wanavyodai; bali kuna vyanzo mbalimbali ikiwamo mtazamo wa mjifunzaji, wasiwasi, mbinu za ufundishaji na hali ya kisaikolojia ya mjifunzaji wa lugha mwenyewe. Nadharia inachunguza mambo makuu manne:

- a. Jinsi mjifunzaji lugha anavyoelewa lugha.
- b. Jinsi mjifunzaji lugha anavyojifunza lugha.
- c. Matatizo anayokabiliana nayo wakati wa kujifunza lugha ya pili au Lgn.
- d. Kung'amua mchakato wa ujifunzaji.

Baada ya uchunguzi wa kina wa hoja hizi, wanausasanyuzi dosari wakiongozwa na Corder (katajwa) wanahitimisha kuwa, dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa lugha ya pili au Lgn hazisababishwi pekee na athari za lugha ya kwanza. Aidha, usasanyuzi dosari umegawika katika matawi mawili: kiunzi cha usasanyuzi dosari na kiunzi cha usasanyuzi tumizi wa dosari.

### **3.1 Kiunzi cha Usasanyuzi Dosari**

Hiki ni kiunzi kinachojaribu kutafuta na kupambanua matatizo mbalimbali yanayohusiana na ujifunzaji lugha. Pia, kinatalii miundo na mifumo inayofanya kazi katika mchakato wa kujifunza lugha. Kadhalika, kiunzi hiki kinachunguza sababu ya dosari katika mchakato wa ujifunzaji. Aidha, kinajihusisha na kubainisha aina ya wajifunzaji lugha, ambao wanategemewa kufanya dosari ikilinganishwa na wajifunzaji wengine. Kwa kuzingatia aina ya wajifunzaji, ilihitimishwa kwamba watu wazima wanaojifunza lugha wana uwezekano mkubwa wa kufanya dosari kuliko watoto wadogo kwa sababu ya mwingiliano baina ya Lugha ya kwanza dhidi ya ile wajifunzayo.

#### **3.1.2 Usasanyuzi tumizi wa dosari**

Hili ni tawi la usasanyuzi linganishi linalojihusisha na utengenezaji wa zana za kujifunzia pamoja na ubunaji wa kozi au masomo ya muda wa ziada. Kwa kifupi, hili ni tawi la usasanyuzi linganishi linalojihusisha na mbinu mbalimbali atumiazo mwalimu kufundisha lugha na jinsi ya kukabiliana na matatizo yenye kuambatana kwayo. Makala haya yanashughulikia dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa Lugha ya pili katika shule za msingi na sekondari nchini Tanzania, jamii ya Wakinga ikitumiwa kama mfano.

#### **4.0 Matokeo ya Utafiti**

Sehemu hii tunawasilisha matokeo ya kuhusiana na dosari zinazojidhihirisha kwa wajifunzaji wa Kiswahili katika jamii ya Wakinga.

#### **4.1 Dosari Zinazofanywa na Wajifunzaji wa Lugha ya pili katika Jamii ya Wakinga**

Lengo mojawapo la utafiti huu lilikuwa-kubainisha dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa lugha ya pili katika jamii ya Wakinga. Katika kufikia lengo hili, mtafiti aliandaa swali la insha, ambalo watoa taarifa waliandika kuhusu shughuli wanazozifanya tangu wanapoamka hadi wanapokwenda kulala. Baada ya kuchanganua insha hizo, dosari kadhaa zilibainika kama zinavyobainishwa katika Jedwali la 1 zilibainika:

#### **Jedwali la 1: Dosari zinazofanywa na Wajifunzaji wa Lugha ya pili katika Jamii ya Wakinga**

<b>Aina za Dosari</b>				
<b>Na .</b>	<b>Dosari za Udondos haji</b>	<b>Dosari za Ubadilishaji wa Fonimu</b>	<b>Dosari za Uchopeka ji</b>	<b>Dosari za Upatanisho wa Sarufi</b>
1.	Øalafu	<i>Lambilamb</i>	Ninamuka	i. ...nasikiliza walimu atasema nini
2.	Lugøa	Mfua	Tunapumu nzika	ii. ...naelekea mstarini, tunafanya usafi
3.	gøarama	<i>fisia</i> gali/lifti		iii. ....mimi ni wanafunzi wa kidato cha pili
4.	gøafla	<i>am/i</i> ya kijiji		iv. ....mwalimu anaturuhusu kuwa niende nyumbani
5.		<i>semanini/s</i>		

		amanini/ <i>fe</i> manini		
--	--	------------------------------	--	--

**Chanzo:** Uwandani (2020)

Kama Jedwali la 1 hapo juu linavyoonesha, wajifunzaji wa Lugha ya pili katika jamii ya Wakinga hufanya dosari mbalimbali. Kuhusu dosari hizi, sehemu zifuatazo zinafafanua kama ifuatavyo:

#### 4.1.1 Dosari za uchopekaji

Dosari ya uchopekaji ni aina ya dosari inayorejelea uongezaji wa umbo fulani la kisarufi au dhana kama vile mofimu, mofu, sauti, au silabi katika mazingira ambamo kipashio hicho hakitakiwi kuwamo. Mfano wa dondoo hapa chini unadhihirisha hali hiyo kwa wajifunzaji wa Lugha ya pili katika jamii ya Wakinga.

**Uchopekaji wa fonimu /-u-/ na /-n-/**

*“NinapoamUka asubuhi kwa sababu mimi ni mwanafunzi ninamUka saa 10:00 kusoma... TunapumUNzika saa nne, tunaingia darasani kusoma. TunapumUNzika saa sita,”*

**Chanzo:** Uwandani (2020)

Dondoo hili ni nukuu kutoka kwenye insha ya mjifunzaji lugha wakati anaeleza shughuli anazofanya kila siku. Fonimu /u/ na /n/ zimeongezwa katika mazingira ambamo hazitarajiwi kuwamo. Kutokana na uongezaji huo, kumetokea kasoro za kifonolojia kulingana na kanuni za Kiswahili sanifu.

#### 4.1.2 Dosari za udondoshaji wa fonimu

Hii ni dosari inayorejelea kuondoa kipashio fulani cha kisarufi katika mazingira ambamo kipashio hicho ni muhimu na kinahitajika ili kukamilisha muundo wa neno husika. Data zilizokusanywa kwa njia ya insha kama dondoo katika 2 zinadhihirisha hali hiyo.

### **Udondoshaji wa fonimu /h-/**

*“...alafu nikitoka kusoma saa 12 ninafanya usafi wa nje na ndani alafu nikishafanya usafi huo naoga, navaa nguo za shule alafu natandika kitanda, nachukua mfuko wa shule naanza kwenda shuleni.*

**Chanzo:** Uwandani (2020)

Kama dondoo katika mfano wa 2 uliopita, mjifunzaji lugha amedondosha fonimu /h-/ katika maneno yaliyoandikwa kwa hati nzito. Udondoshaji wa sauti unasababisha dosari, kwa kuzingatia kanuni za Kiswahili sanifu. Aidha, mifano mingine zaidi ni kama jedwali la 2 hapa chini linavyoonesha.

### **Jedwali la 2: Udondoshaji wa Fonimu /h/**

<b>Neno la Kiswahili sanifu</b>	<b>Udondoshaji wa Fonimu /h/</b>
Halafu	Øalafu
Lugha	Lugøa
Gharama	Gøarama
Ghafla	Gøafla

**Chanzo:** Uwandani (2020)

### **4.1.3 Dosari za ubadilishaji wa fonimu**

Hizi ni dosari zinazotokana na mjifunzaji lugha kutumia fonimu nyingine badala ya ile inayotakiwa, kwa mujibu wa kanuni za Kiswahili sanifu. Uchanganuzi wa insha zilizoandikwa na wajifunzaji wa lugha ya pili ulionesha wajifunzaji wa lugha ya pili wamefanya ubadilishaji wa fonimu mbalimbali kama zinavyooneshwa katika jedwali la 3 hapa chini:

### **Jedwali la 3: Ubadilishaji wa Fonimu**

<b>Na.</b>	<b>Ubadilishaji wa fonimu</b>	<b>Muundo sahihi wa Kiswahili</b>
1.	<i>Lambi/lambi</i>	Rambirambi
2.	<i>Mfua</i>	Mvua
3.	<i>fisia gali/lifti</i>	Vizia gali/lifti
4.	<i>am/i ya Kijiji</i>	Amri ya kijiji
5.	<i>semanini/samanini/femanini</i>	Themanini

**Chanzo:** Uwandani (2020)

Kama Jedwali la 3 linavyoonesha, wajifunzaji wa lugha ya pili wamebadilisha fonimu zinazotakiwa kutumika katika neno husika na kutumia zingine. Matumizi hayo hayakubaliki kulingana na utamkaji wa Kiswahili sanifu. Katika mfano wa 1 na 4 katika jedwali, mjifunzaji ametumia fonimu /l/ badala ya fonimu /r/. Katika mfano wa 2, mjifunzaji amebadilisha fonimu /v/ na kutumia /f/. Aidha, katika mfano wa 5 mjifunzaji lugha amebadili fonimu /ø/ na kutumia fonimu /s/ na /f/. Hali hiyo imesababisha dosari za kifonolojia kwa kuzingatia kanuni za sarufi ya Kiswahili.

#### **4.1.4 Dosari za upatanisho wa sarufi**

Hizi ni dosari zinazotokana na mpangilio mbaya wa maneno katika sentensi au tungo. Katika uchanganuzi wa insha zilizoandikwa na wajifunzaji wa lugha ya pili katika jamii ya Wakinga, imebainika kuwa wajifunzaji lugha hawa hushindwa kupangilia tungo zenye zinazowiana. Kwa mfano, wajifunzaji wa lugha ya pili katika jamii ya Wakinga hufanya dosari za kuoanisha mpangilio wa maneno katika tungo. Katika uchunguzi uliofanyika kwenye insha za wajifunzaji wa lugha ya pili, ilibainika wajifunzaji lugha kutunga sentensi ambazo hazina upatanisho wa kisarufi kama mifano ifuatayo inavyoonesho:

### **Dosari za Upatanisho wa Sarufi**

- i. "...nasikiliza **walimu** atasema nini"
- ii. "...**Mimi** ni wanafunzi wa kidato cha pili"
- iii. "...**ninaelekea** mstarini, **tunafanya** usafi"
- iv. "...mwalimu anaturuhusu kuwa niende nyumbani"

**Chanzo:** Uwandani (2020)

Kama tungo zinavyoonesha, kuna kasoro za upatanisho wa kisarufi. Katika tungo ya 3 i-iv) wajifunzaji lugha wamechanganya wingi na umoja. Kwa mfano, nomino *mwalimu* haichukui kipatanishi *a-* kama ilivyo katika dondoo. Kadhalika, kiwakilishi mimi, ambacho ni kiima cha tungo ya pili, hakichukui kipatanishi *wa-*. Vilevile, tungo ya 3 (iii), kipatanishi **ni-** katika kitenzi **ninaelekea** mstarini si sahihi kwenda na kipatanishi **tu-** katika neno **tunafanya** usafi. Kama ilivyodokezwa hapo awali, tungo hizo zimedondolewa kutoka kwenye insha za wajifunzaji wa Lugha ya pili katika jamii ya Wakinga. Aidha, kimuundo, tungo hizi hazikubaliki, kwa mujibu wa kanuni za Lugha ya pili sanifu, kwa kuwa kila tungo ina dosari.

### **4.2 Sababu za Dosari kwa Wajifunzaji wa Lugha ya Pili katika Jamii ya Wakinga**

Mingoni mwa malengo mahususi ya makala haya ni kufafanua sababu za dosari za wajifunzaji wa Lugha ya pili katika jamii ya Wakinga. Katika kuhakikisha lengo hili linafikiwa, watoa taarifa, ambao ni walimu wa shule za msingi na sekondari, walijaza hojaji. Uchunguzi uliofanywa na makala haya kwa njia ya hojaji ulibaini sababu zifuatazo kuwa ndizo zinazosababisha hali ya dosari kwa wajifunzaji wa Lugha ya pili katika jamii ya Wakinga kama zinavyooneshwa katika Jedwali la 4.

#### **Jedwali la 4: Sababu za Dosari kwa Wajifunzaji wa Lugha ya pili**

<b>Na.</b>	<b>Sababu za Dosari kwa Wajifunzaji wa Lugha ya pili</b>
1.	Athari za Lugha mama/Kikinga
2.	Ukosefu wa mwingiliano baina ya Wakinga na jamii nyingine
3.	Tofauti ya Kikinga na Kiswahili
4.	Kuchelewa kuanza kujifunza Kiswahili miongoni mwa Wakinga
5.	Mazingira hayawezeshi ujifunzaji wa Kiswahili
6.	Tofauti ya kimsamiati kati ya Kikinga na Kiswahili

**Chanzo:** Uwandani (2020)

Kama Jedwali la 4 linavyoonesha, sababu za dosari miongoni mwa wajifunzaji wa Lugha ya pili ni nyingi. Kwanza kabisa ni athari za lugha mama/Kikinga. Dosari za wajifunzaji wa lugha zinasababishwa na athari za lugha ya kwanza. Hii ina maana kwamba, mazoea ya kutumia lugha ya Kikinga ndiyo hufanya wahamishe kanuni za lugha ya Kikinga na kuingiza katika lugha ya pili. Uchunguzi uliofanywa na mtafiti wa Makala haya unaonesha kwamba, wajifunzaji wa lugha ya pili muda mwingi wakiwa nyumbani pamoja na wazazi na walezi wao hutumia lugha ya Kikinga tu katika kufanya mawasiliano. Mazoea haya huwafanya wajifunzaji lugha hawa kuhawilisha utaratibu wa lugha ya Kikinga katika Kiswahili. Kwa kufanya hivyo, dosari hutokea kwa kuzingatia ukiushi wa taratibu za Kiswahili sanifu.

Pili, ni tofauti za kimofolojia na kifonolojia kati ya Kikinga na Kiswahili. Kimatamshi, lugha ya Kikinga ni lugha yenye toni, ilhali Kiswahili ni lugha ya mkazo. Hivyo, mjifunzaji anapotumia kanuni za lugha ya kwanza katika lugha ya pili huleta miundo isiyokubalika. Vilevile, kukosekana kwa baadhi ya sauti katika lugha ya pili, ambazo zimo katika Kikinga ni chanzo kingine cha dosari za wajifunzaji wa lugha ya pili. Kwa mfano, sauti /e/ na /š/ hazimo katika mfumo wa lugha ya Kikinga lakini



zimo katika sarufi ya Kiswahili. Hivyo, wajifunzaji kila wanapokutana na sauti hizi hupata ugumu wa kuzitumia katika lugha ya pili.

Tatu, ukosefu wa mwingiliano na jamii nyingine kutoka nje ya maeneo ya utafiti. Katika eneo ambalo uchunguzi ulifanywa ni eneo lenye milima, baridi kali na miundo mbinu kama vile barabara, umeme na maji kuwa duni. Mambo haya kwa ujumla yanatatiza maingiliano ya jamii kutoka nje ya Wilaya ya Makete. Katika shule ambamo utafiti ulifanyika, wajifunzaji lugha ni wenyeji wa Makete tu. Ukosefu wa mwingiliano, huwafanya wajifunzaji wa Lugha ya pili muda mwingi kutumia Lugha ya kwanza hata katika mazingira ya shule. Maelezo haya yanashabihana na matokeo ya Gawasike (2016) anaposema kwamba, licha ya kuwapo kwa miongozo ya matumizi ya Kiswahili katika mazingira ya shule, bado wajifunzaji hutumia lugha ya Kikinga. Hiki ni chanzo kingine cha dosari kwa wajifunzaji wa Kiswahili katika jamii ya Wakinga.

Nne, kuchelewa kuanza kujifunza lugha ya pili miongoni mwa wanajamii wa Kikinga. Uchunguzi uliofanywa na mtafiti wa makala haya umebaini kwamba, asilimia 78 ya wajifunzaji wa Lugha ya pili, huanza kujifunza lugha ya pili wakiwa na umri kati ya miaka 6 mpaka 10. Ni asilimia 22 tu ndiyo huanza kujifunza Kiswahili kabla ya kufika umri wa miaka 6. Katika wakati huo, yaani kabla ya miaka 6 mpaka 10 lugha inayotumika ni Kikinga tu. Katika umri huo, mifumo ya lugha ya Kikinga huwa umejengeka sana, miongoni mwa wajifunzaji hawa kiasi cha kuwawia vigumu kupokea mifumo mingine ya lugha kutokana na mazoea ya kutumia lugha ya Kikinga zaidi kuliko Kiswahili. Uchunguzi unaonesha kwamba, asilimia 80.5 ya wajifunzaji hutumia Kikinga wakiwa mazingira ya nyumbani. Hata hivyo, ni asilimia 19.5 ya wajifunzaji lugha pekee inayochanganya Kiswahili na Kiingereza wawapo nyumbani.

Tano, mazingira hayawezeishi kujifunza lugha ya pili. Hii ina maana kwamba, wajifunzaji wa lugha ya pili wanazungukwa na wazungumzaji wa Kikinga tu. Yaani, wazazi na walezi hutumia lugha ya Kikinga zaidi kuliko Kiswahili. Jambo, hili huwafanya wajifunzaji lugha hawa kukosa ingizo huria. Yaani hawasikii lugha ya pili nje ya mazingira ya shule. Kwa hiyo, ukosefu wa ingizo la kutosha kutoka katika mazingira ya kijamii ni chanzo kimojawapo cha dosari za wajifunzaji wa lugha ya pili katika jamii ya Wakinga.

#### **4.3 Mbinu Zinaweza Kutumika Kupunguza Dosari**

Lengo la tatu la makala haya lilikuwa kupendekeza mikakati inayoweza kutumika ili kupunguza dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa lugha ya pili katika jamii ya Wakinga. Katika kutimiza lengo, iliandaliwa hojaji kwa ajili ya walimu wanaofundisha Kiswahili katika jamii ya Wakinga. Swali lifuatalo lilitumika kudodosa, *“Je unafikiri ni mbinu gani zinaweza kutumika ili kuwasaidia wanafunzi wa Kiswahili katika jamii ya Wakinga kumudu vizuri lugha ya pili.”* Majibu kutokana na swali hili ni kama inavyooneshwa katika jedwali la 5.

#### **Jedwali la 5: Mbinu za Kupunguza Dosari**

<b>Na.</b>	<b>Mbinu iliyopendekezwa</b>
1.	Shule za awali zijengwe/watoto wafundishwe wangali wadogo
2.	Kuboresha miundombinu ili kuruhusu mwingiliano
3.	Kuwapo kwa midahalo ya kwa Kiswahili
4.	Wataalamu/walimu wa Kiswahili wenye sifa waletwe

**Chanzo:** Uwandani (2020)

Kama Jedwali la 5 linavyoonesha, mbinu mbalimbali zinapendekezwa ili kupunguza dosari za wajifunzaji wa lugha ya pili. Pendekezo la kwanza ni kujengwa kwa shule za awali. Katika shule za awali, watoto wadogo

watafundishwa lugha ya pili, kabla mifumo ya lugha ya kwanza haijaimarika miongoni mwa watoto hao. Hali hii itasaidia kuepuka wajifunzaji lugha ya pili kukakamaa. Zipo nadharia zinazoshadidia mwingiliano wa kijamii na nafasi yake katika kujifunza lugha ya pili kama vile nadharia ya Utabia ya Skinner (1957) na Nadharia ya Maingiliano ya Kijamii Vygostky (1978).

Hata hivyo, ili mawazo ya nadharia hizi yaweze kufanya kazi na kumsaidia mjifunzaji lugha ya pili kumudu lugha anayojifunzi shurti jamii inayomzunguka mjifunzaji lugha husika ziwe zinatumia lugha hiyo kuwasiliana katika mazingira yao ya kila siku. Kutumia lugha hiyo kuwasiliana wawapo nyumbani na katika shughuli nyingine za kijamii ili kumwezesha mjifunzaji lugha huyu kuamili lugha hiyo kwa njia ya uigaji au mwigo. Katika mazingira ya wajifunzaji lugha ya pili katika jamii ya Wakinga, hali haiko hivyo. Wazawa wa eneo la utafiti hutumia lugha ya Kikinga katika mawasiliano karibu yote. Mjifunzaji lugha ya pili anapotoka nje ya mazingira ya hukutana na Kikinga katika mawasiliano yao ya kila siku. Kinadharia, umri sahihi wa kujifunza na kumudu lugha ni ule umri wa kabla ya balehe (Lenneberg, 1967; Penfield & Roberts, 1959).

Pili, kuboresha miundombinu ili kuruhusu mwingiliano. Miongoni mwa sababu za dosari imebainika kuwa ni kukosekana kwa maingiliano na wanajamii wengine ya Wilaya ya Makete. Hivyo, miundombinu ya barabara, umeme na maji ikiboreshwa, watu kutoka nje ya Wilaya ya Makete watakwenda kufanya kazi huko kama manesi na walimu, hivyo, mwingiliano na jamii nyingine utakuwa unatokeo na hivyo kuleta mabadiliko ya kutumia lugha. Watoto wa jamii ya Wakinga watalazimika kuzungumza Kiswahili na wenzao ambao hawajui Kikinga. Kwa sasa,

wafanyakazi wengi wanapopangiwa maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Makete huomba kuhamishwa, na baadhi ya wafanyakazi hawaripoti kabisa vituoni kwao.

Tatu, kuwepo midahalo itakayotumia lugha ya Kiswahili. Hali hii itawalazimu wajifunzaji Kiswahili kukitumia mara kwa mara. Matokeo yake, ndimi zao zitajizoesha kuzungumza lugha ya Kiswahili tofauti na ilivyo sasa, ambapo Kiingereza kinahamasishwa Zaidi na kutumiwa na wajifunzaji Kiswahili kama lugha ya pili. Mwisho, wataalamu wa Kiswahili wenye sifa wapelekwe kufundisha Kiswahili katika maeneo haya. Uchunguzi uliofanywa na mtafiti wa makala haya, umebaini kuwa walimu wengi wanaofundisha Kiswahili katika shule zilizofanyiwa utafiti, hawana mafunzo ya ufundishaji wa lugha ya pili. Zaidi, hawana ufahamu ikiwa Kiswahili ni lugha ya pili katika maeneo zilizomo shule zao. Jambo hili linawafanya walimu hao kufundisha Kiswahili kama masomo mengine. Hivyo, kupeleka walimu wenye mafunzo ya mbinu za ufundishaji wa Kiswahili ikiwa ni lugha ya Kigeni kunaweza kusaidia kupunguza dosari zinazofanywa na wajifunzaji lugha hawa.

#### **4.0 Hitimisho na Mapendekezo**

Makala haya yanahusu dhima ya usasanyuzi dosari katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili katika jamii ya Wakinga. Data zilikusanywa kwa wajifunzaji lugha kwa njia mbili: uandishi wa insha na hojaji. Nadharia ya Usasanyuzi Dosari ya Corder (1967, 1974) iliongoza utafiti huu. Matokeo yameonesha kuwa wajifunzaji lugha hufanya dosari za: udondoshaji wa fonimu, uchopekaji fonimu, ubadilishaji fonimu na dosari za ukosefu wa upatanisho wa kisarufi. Pia, sababu za dosari zimebainishwa kuwa ni athari za lugha ya kwanza, tofauti za kimofolojia kati ya lugha ya kwanza na lugha ya pili, kuchelewa kuanza kujifunza

lugha ya pili na mazingira yasiyoweza kujifunza lugha ya pili. Mikakati anuai imependekezwa ili kupunguza dosari hizo kama vile: shule za awali zijengwe/watoto wafundishwe wangali wadogo, kuboresha miundombinu ili kuruhusu mwingiliano, kuwapo kwa midahalo ya kwa Kiswahili na wataalamu/walimu wa Kiswahili wenye sifa waletwe. Hivyo, usasanyuzi dosari unatumika kama chombo cha kuonesha welewa mpana wa jinsi mchakato wa ujifunzaji wa Lugha ya pili ulivyo pamoja na changamoto zinazowakabili wajifunzaji wa lugha.

### **Marejeleo**

Corder, S. P. (1967). The significance of learners' errors. *Int. Rev. Appl. Linguist.*, 5, 161–169.

Corder, S. P. (1971). *Idiosyncratic dialects and error analysis* (uk.14). Groos, Heidelberg. <http://dx.doi.org/10.1515/iral.1971.9.2.147>.

Corder, S. P. (1974). *Error analysis*. Katika J. P. B. Allen, na S. Pit Corder (Wah.), *Techniques in Applied Linguistics*. London: Oxford University Press.

Darus, S. (2009). Error analysis of the written English essays of secondary school students in Malaysia: A case study. *Eur. J. Soc. Sci.*, 8(3), 483–495.

Ellis, R. (1995). *Understanding second language acquisition*. Oxford: Oxford University Press.

Gawasike, A. (2016). *Ukakamaaji kwa wajifunzaji wa Lugha ya pili katika jamii ya Wakinga*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapwa): Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Gass, S. M., & Selinker, L. (2008). *Second language acquisition: An introductory course*. New York and London: Routledge.

- James, C. (1989). *Contrastive analysis*. London: Longman.
- James, C. (1998). *Errors in language learning and use*. London: Longman.
- Kazemian, B., & Hashemi, S. (2014). A contrastive linguistic analysis of inflectional bound morphemes of English, Azerbaijani and Persian languages: A comparative study. *Journal of Education & Human Development*, 3(1), 593–614.
- Keshavarz, M. H. (2003). *Contrastive analysis and error analysis*. Tehran: Rahnama Publications.
- Keshavarz, M. H. (2006). *Error analysis: A practical course for English students and teachers*. SAMT, Tehran.
- Lenneberg, E. (1967). *Biological Foundations of Language*. New York: Wiley.
- Norrish, J. (1983). *Language learners and their errors*. London: Macmillan Publishers.
- Penfield, W., na Robert, L (1959). *Speech and Brain Mechanism*. New York: Atheneum.
- Richards, J. C. (1971). A noun-contrastive approach to error analysis. *English Language Teaching*, 25(3), 204–219. <http://dx.doi.org/10.1093/elt/XXV.3.20>.
- Richards, J. (1974). *Error analysis and second language strategies*. Longman.
- Şanal, F. (2007). *A learner-based study on second language lexicology of Turkish students of English*. Tasnifu ya Uzamivu. Haijachapwa: Çukurova University.

- Skinner, B. F. (1957). *Verbal behaviour*. New York: Appleton-Century-Crofts.
- Vygotsky, L. S. (1978). *Mind in Society: The Development of Higher Psychological Processes*. London: Harvard University Press.
- Wei, X. (2008). Implication of IL Fossilization in Second Language Acquisition. *Katika English Language Teaching*. Juzuu 1, China: Beijing Language and Culture University.
- Ziahosseiny, S. M. (1999). *A contrastive analysis of Persian and English and error analysis*. Tehran: Nashr-e Vira.